Fidia ya majeraha yatokanayo na uhalifu

Criminal Injuries Compensation - Swahili

Sheria ya fidia kwa majeraha ya uhalifu

Iwapo umejeruhiwa au kuteseka hasara kutokana na tuhuma za uharifu unaweza kutoa madai ya fidia chini ya sheria ya 2003 ya fidia dhidi uarifu (WA) (sheria). Sheria ni tata katika eneo hili na inasisitizwa sana kwamba unapaswa kutafuta msaada wa kisheria iwapo tu unahakika kwamba una malalamiko yanayo hitaji fidia ya kujeruhiwa katika uhalifu.

Lalamiko linaweza kutolewa kwa ajili ya kupatiwa fidia ya madhala na / au upotevu uliosababishwa na shitaka ambalo limefanyika au baada ya tarehe 22 Januari 1971. Kiasi cha juu cha fidia ya kuumizwa inayoweza kulipwa kwa muathirika kwa sasa ni dola za Australia 75,000.00, kutegemea na lini shitaka lilitokea.

Nani anaweza kutoa madai?

Ni mwathirika wa tuhuma na waakati mwingine ndugu wa karibu wanaweza kuleta madai ya fidia ya kujeruhiwa katika uharifu chini ya sheria hii. Tafsiri ya ndugu wa karibu imetolewa na sheria hii na inawajumuisha kwa mfano, wazazi, babu na bibi, mwenza au mototo. Haiwajumuisha kaka na dada.

Mwathirika au ndugu wa karibu bado anaweza kutoa madai hata kama mtuhumiwa hajakamatwa au hajathibitika. Hii inategemea mazingira fulani fulani.

Mtu ambaye hamjui mwathirika anaweza kutoa madai ya fidia katika hali ambapo watabaini mshtuko wa ufahamu au akili, iwapo watakutwa katika eneo la tukio wakati kosa linatokea au katika eneo la tukio mara tu baadaye, na watashuhudia mtu kujeruhiwa au kuuwawa kama matokeo ya tuhuma.

Nini kinaweza kudaiwa?

Waathirika wa kosa wanaweza kudai kwa majeraha na / au upotevu waliyoupata.

Majeraha yatajumuisha kuumizwa kimwili,kiakili, mshituko wa ufahamu au ujauzito . Waathirika pia wanaweza kudai kwa upotevu kama vile maumivu na kusumbuliwa, upotevu wa kipato na gharama ambazo kwa hakika zimempata kutokana najeraha.

Ndugu wa karibu wanaweza kutoa madai ya fidia endapo mwathirika amefariki au amejeruhiwa kisaikorojia kutokana na tukio. Madai ya namna hii yanaweza kujumuisha fidia kwa ajili ya gharama za mazishi, kuondokewa kwa msaada wa kifedha kwa wategemezi na mshtuko wa kiakili na ufahamu

Unaweza kudai gharama za matibabu zinazotarajiwa iwapo daktari wa meno au msaikolojia atathibitisha kwamba utahitaji matibabu zaidi hapo baadaye. Kuna mashrti ili kupata gharama ya matibau hayo na iwapo gharama hazitalipwa mpaka upatiwe matibabu hayo.

Nini mwathirika wa uhalifu atatakiwa kufanya mara baada ya uhalifu?

Kama wewe ni mwathirika wa uharifu utapaswa kuripoti uharifu huo kwa polisi mapema iwezekanavyo na utoe taarifa zote ambazo zinaweza kuhusiana na tukio. Unaweza kutokubaliwa kulipwa fidia au fidia inawezwa kupunguzwa iwapo hatatoa

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo tu wa jumula na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, Case kwa wakimbizi Inc. Inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomaji lazima apate ushauri wa kisheria maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.

ushirikiano wa kutosha wa kipolisi katika uchungu wao.

Kufanya madai ya fidia

Maombi ya fidia ya majeraha ya uharifu yanafanyika kwenye ofisi ya fidia ya majeraha ya uharifu. Kwa sasa hakuna ada ya kujaza maombi.

Maombi haya yatajumuisha idadi kadhaa ya vielelezo, ikiwa ni pamoja na taarifa ya matibabu,vithibitisho vya gharama kama vile gharama za matibabu, gharama za usafiri na mzishi na taarifa yako ya maandishi kuhusu jeraha na/au upotevu ulivyo na jinsi ulivyo athirika . Kwa mfano, kama utapoteza uwezo wa kufanya kazi, utapaswa kueleza katika taarifa yako. CASE kwa wakimbizi Inc. itaweza kukusaidia kukamilisha maombi yako.

Maombi ya fidia kikomo chake ni miaka mitatu tangu uhalifu ufanyike au tangu tarehe ya tuhuma ya mwisho ambapo kuna mlolongo wa tuhuma kwa mtuhumiwa huyo huyo. Muda wa kikomo unaweza kurefushwa kadri ofisi ya fidia ya majeruhi ya urefu itakavyo amua kufanya hivyo

Malipo ya mda

Madai ya malipo ya muda ni madai ya mbele kwa malipo au kurudishiwa gharama ikiwa ni matokeo yatokanayo na madhara kabla maombi ya kawaida hayajashughulikiwa. Madai ya malipo ya muda yanaweza kufanywa muda wowote baada ya ajari. Unaweza kudai malipo ya mda kwa:

- baadhi ya matibabu na gharama za ripoti
- Garama za usafiri; na
- Garama za mazishi

Malipo ya muda yanakuwa kama sehemu ya fidia utakayopewa. Kama madai ya fidia yamekataliwa, basi malipo ya muda inakuwa ni deni ambalo lazima ilipwe kwa utawala wa mkoa.

Njia nyingine za kupata fidia kama mwathirika wa uhalifu

Unaweza pia kupewa mamlaka ya kutumia sheria ya kawaida ya madai ya fidia ya jeraha au hasara au pale mtuhumiwa anapo shitakiwa, kutumia maombi kwa mahakama kumhukumu mtuhumiwa kulipa fidia. Kuna faida na hasara kwa njia zote za kufanya madai ya fidia na utapaswa kupata ushauri wa mwanasheria kabla ya kufanya madai.

Wapi pa kupata masaada?

CASE kwa wakimbizi inc. ni taasisi isiyo ya kiserikali au kidini ambayo inasaidia wahamiaji na shughuli zote za kisheria katika mila na isimu ya Lugha(Cald)katika jamii ya Australia Magharibi. CASE kwa wakimbizi inc. inaweza kukusaidia kwa ushauri utokanao na malalamiko ya fidia ya majeraha yatokanayo na uharifu.

Huduma zote sio za malipo, ingawa misaada ya watu binafsi na mashirika inapokelewa kwa ukarimu. Michango yote ya zaidi ya AUD $2.00 haina vati.

Mawasiliano ya CASE kwa wakimbizi inc.ni haya yafuatayo :

145 Stirling Street, Perth
Western Australia 6000
Simu:(08) 92277311
Kinukushi: (08) 92277188

Email: admin@caseforrefugees.org.au

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo tu wa jumula na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, Case kwa wakimbizi Inc. Inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomaji lazima apate ushauri wa kisheria maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.